# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SITA

## KIKAO CHA KUMI NA TATU

**17 FEBRUARI, 2022**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA SITA

### KIKAO CHA KUMI NA TATU – TAREHE 17 FEBRUARI, 2022

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Mapendekezo ya Nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022**.**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

## III. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**149. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kiwango cha mkopo wa 10% kwa Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu.

**150. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Afya eneo la Nsemulwa na Mwamkulu katika Manispaa ya Mpanda.

**151. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza ukarabati wa Shule za Msingi kongwe ambazo zimechakaa.

## WIZARA YA AFYA:

**152. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itakabidhi majengo yaliyokuwa ya Hospitali ya Muhimbili kwa Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo ili kupunguza uhaba wa majengo katika Hospitali hiyo.

## WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

**153. MHESHIMIWA MWANTUM DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia akina Mama wafanyabiashara ili wafanye biashara zenye tija.

## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**154. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, nini kauli ya Serikali kutokana na mkanganyiko uliotokea kuhusu fidia katika Barabara ya Tanga – Pangani.

**155. MHESHIMIWA KHAMIS MBAROUK AMOUR (TUMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali inakusanyaje ushuru kwenye Boti zinazoondoka saa moja kamili asubuhi katika Bandari ya Dar es Salaam ilihali Watumishi hufika kazini kuanzia saa moja na nusu na zaidi.

**WIZARA YA MAJI:**

**156. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuhakikisha kwamba maji yote yaliyopo ardhini yanabaki salama kwa kuwa tone moja la oil (vilainishi) huharibu lita 600 za maji yaliyoko ardhini.

**157. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itasambaza maji katika Vijiji vya Mwanjoro, Jinamo, Mbushi na Witamihya Wilayani Meatu baada ya ujenzi wa Bwawa la Mwanjoro kukamilika.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**158. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMEDI KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya udanganyifu kwenye Mikataba ya ushuru wa Kampuni za Simu na wenye maeneo yanayojengwa minara ya simu kiasi cha kusababisha ushuru kwenda kwa watu wasiohusika.

**IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

## V. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

**DODOMA**
**17 FEBRUARI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**